OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

MKOA WA DAR-ES-SALAAM

MUONGOZO WA USAHIHISHAJI WA MTIHANI WA UTAMILIFU DAR-ES-SALAAM.

KIDATO CHA SITA. 2025.

KISWAHILI 1.

1. Mwanafunzi atajibu swali la ufahamu kama ifuatavyo.

a/. HADITHI YA SHUJAA MKOMBOZI (Alama 1)

b/. faida

i/. aliwakomboa wanajamii kutokana na hujuma za majitu mawili.

ii/. alikuwa na upendo kwani alimpenda chakisasi pasipo kujua hakuwa binadamu wa kawaida. (Alam: 1@2)

c/. Sifa za chakisasi

i/. Alikuwa mwanamke mrembo sana "kipusa"

ii/. Hakuwa binadamu wa kawaida. (Alama 1@2)

d/. Msemo huu "Nifae juani, nikufae mvuani" katika maisha unaweza kumsaidia mtu usiyemjua, kwani huwezi jua ipo siku atakufaa kwa namna nyingine usiyotegemea. (alama 1)

e/. Neno "jitu" limetumika katika hali ya ukubwa

f/. Maana ya msamiati

i/. Lilinusurika - kuepuka madhara makubwa kama kifo au kuponea chupuchupu.

ii/. Nasua - ondoa au toa mtegoni kitu kilichonaswa.

iii/. Kipusa - Msichana au mwanamke mrembo

iv/. Makinda - vitoto vichanga/vidogo vya ndege

v/. Hujuma - shambulio, vamio, vuruga au kuharibu

vi/. Vurumai - hali ya kutosikilizana, fujo, zogo, ghasia, vurugu nk.

(alama ½ @ 6)

Jumla alama 10

2. Mwanafunzi kwa kutumia mifano aelezee maana ya maneno yafuatayo kama ifuatavyo

a/. Mzizi – ni sehemu ya neno ambayo haibadiliki baada ya kuondolewa viambishi awali na tamati
Mf. lim, pik, andik nk.

b/. Kishazi tegemezi – Ni kishazi ambacho hakitoi taarifa kamili kutokana na kiterzi kushushwa hadhi na kutegemea kishazi huru ili kukamilika maana yake.
Mf. Aliyepoteajana
ktg (r)

c/. Vimadende – Ni sauti ya lugha inayotamkwa kwa kupigapiga ulimi harakaharaka. Sauti hii inawakilishwa na herufi "r" katika alfabeti ya kiswahili

d/. Alomofu – Ni maumbo zaidi ya moja yenye kuwakilisha mofimu moja kisarufi.

Mf. anal ima
alilima
atalima
amelima

∴ na, li, ta na me ni alomofu za wakati

e/. Shamirisho
Ni sehemu ya kiarifu inayokaliwa na nomino (yambwa au kikundi nomino) katika sentensi.
Mf. Mtoto anakula chakula
sh.

(Alama 2@5 Jumla 10)

3. Mwanafunzi aoneshe tofauti kati ya mofimu tegemezi na silabi katika Lugha ya Kiswahili.

i/. Viambishi - Katika mofimu tegemezi kuna viambishi mbalimbali kama viambishi vya nafsi, wakati, idadi nk.

ii/. Maana - Mofimu tegemezi ni aina ya mofimu isiyosimama pekeyake na kuleta maana ya neno/kitenzi ibyokamilika.

iii/. Mzizi/shina katika mofimu kuna mzizi/shina la neno lakini katika silabi hakuna mzizi au shina la neno.

iv/. idadi - Mofimu tegemezi ina idadi chache lakini silabi ina idadi nyingi

v/. Kazi za viambishi - kila mofimu ina kazi kisarufi mf. kuonesha urejeshi, umoja nk lakini umbo la silabi moja halina kazi ya kisarufi

vi/. Uvunjwaji - Mofimu tegemezi inaweza kuvunjwavunjwa kutoka kwa neno, mpaka mzizi na viambishi tamati lakini silabi haiwezi kuvunjavunja

vii) Aina

2 @ 5 jumla alama 10

04. Mtahiniwa aelezee kwa ufupi Sifa tano (5) za mtindo wa Lugha wa kitaaluma.

i/. Mada inayozungumzwa au kuandikwa ni ya kitaaluma.

ii/. kuna usahihi na ukweli wa mambo yanayojadiliwa.

iii/. Hutumia kauli ya kutendwa na kutendeka kwa wingi zaidi.

iv/. Hutumia lugha sanifu ya wazi na inayoeleweka.

v/. Hakuna matumizi ya tamathali za semi au nafumbo isipokuwa kwa kazi za kifasihi.

vi/. Kuna ufupishaji maalum wa maneno

vii/. Hutumia wakati uliopita hasa katika uandishi wa ripoti

viii/. Hutumia istilahi maalum kulingana na uwanja husika

(alama 2@5)

05. (a) Mwanafunzi aeleze vikwazo ambavyo mfasiri hukutana navyo katika kazi ya tafsiri.

i/. Tofauti za kiisimu

ii/. Tofauti za mitindo

iii/. Tofauti za kiutamaduni

iv/. Tofauti za kidini (kiitikadi)

v/. Tofauti za matumizi ya lugha (ugumu wa kutafsiri misemo, nahau au semi mbalimbali za Kiswahili)

{ Alama utangulizi 3
kiini 10
Hitimisho 2 }

(b). TANZANIA NATIONAL ANTHEM

God bless Tanzania
Bless her leaders
Let wisdom, unity and peace
God bless Tanzania
God bless Tanzania
Bless the children of Tanzania.

{Alama 5}

(Jumla Alama 20)

06. Swali linamtaka mwanafunzi afafanue idara tano (5)

Utangulizi - Aeleze bakita ni nini imeanzishwa (alama 3)

Kiini

- Idara za BAKITA na kazi zake kwa ufupi

i/. idara ya ushairi na uchapishaji

ii/. idara ya lugha na fasihi

iii/. Idara ya Tafsiri na ukalimani

iv/. Idara ya Istilahi na Kamusi

v/. idara ya mawasiliano

(3@5 jumla 15)

Hitimisho alama 2

07. Mtahiniwa aeleze maana na muundo wa wasifu kisha aandike wasifu wa kazi kama inavyoelekezwa na swali.

Wasifu wa kazi ni maelezo yanayotoa taarifa za mtu binafsi zinazojumuisha mahali anapoishi, tarehe ya kuzaliwa, usuli wa elimu, uzoefu wa kazi, raghba, ujuzi, wadhamini na mawasiliano yake ambayo huambatana na barua ya kuomba ajira au kujitambulisha mahali fulani (Alama 02)

Muundo wa wasifu kazi

i/. Taarifa binafsi

ii/. Usuli wa elimu

iii/. Uzoefu wa kazi

iv/. majina ya wadhamini

(alama 2@4 jumla 8)

# WASIFU WA KAZI (alama 2)

1.0 Taarifa Binafsi

Jina la Ukoo:

Majina mengine:

Tarehe ya Kuzaliwa:

Uraia:

Jinsia:

Hali ya ndoa:

Lugha:

Anwani:

Simu:

Barua pepe

(alama 2)

2.0 Usuli wa Elimu (alama 2)

| Mwaka | Kiwango cha Elimu | Shule | Tuzo |
|---|---|---|---|
| 2007-2010 | chuo kikuu | UDOM | cheti cha kuhitimu elimu ya juu |
| 2005-2007 | Elimu ya juu sekondari | Shule ya sekondari Mwembeni | cheti cha kuhitimu kidato cha sita |
| 2001-2004 | Elimu ya sekondari | Shule ya sekondari Kibara | cheti cha kuhitimu kidato cha nne |
| 1994-2000 | Elimu ya msingi | Shule ya msingi Mazoezi-Bunda | cheti cha kuhitimu darasa la saba. |

3.0 Uzoefu wa kazi (alama 2)

| Mwaka | Kazi/shughuli | wadhifa | Mahali |
|---|---|---|---|
| 2011-2012 | kuuza vifaa vya elimu. | meneja masoko | Kampuni ya Elimika |
| 2004-2005 | fundi wa kutengeneza nguo | fundi | A-Z Arusha |

4.0 Wadhamini (alama 2)

8. Mwanafunzi aelezee maana, umuhimu na hatua za Usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili

Utangulizi – Maana ya Usanifishaji (Alama 1)

Kiini

Umuhimu wa Usanifishaji

- Kutambulisha utamaduni wa jamii husika
- Lugha kutumika kwa namna moja
- Kuondoa tofauti za kikabila

nk 3@1 = 3

Hatua

- Uteuzi wa lahaja
- Kuunda kamati ya Lugha
- Kukubaliana kuhusu mfumo wa kisanifi
- Kutoa machapisho
- Kuandaa wataalamu wa Usanifishaji

(2@3 = 15

Hitimisho 01

(Jumla Alama 20.)